

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA NANE

13 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA NANE – TAREHE 13 APRILI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhhibiti wa UKIMWI) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

60. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ipo tayari kuruhusu Wananchi wanaoishi kwenye Miji ambayo ipo kando ya barabara kuu kama Mji wa Mafinga kufanya biashara kwa saa ishirini na nne.

61. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya kujaa maji mara tu mvua zinaponyesha katika baadhi ya maeneo ya Kata za Magomeni, Shangani, Ufukoni, Reli na Likombe katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

62. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi ya mabasi ya Mji wa Katesh.

WIZARA YA MAJI:

63. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupima na kuchimba visima virefu Mkoani Arusha hasa Wilaya ya Longido katika Vijiji vya Noondoto, Matale, Wosiwosi na Ngereani ambapo kuna uhaba wa vyanzo vya maji safi na salama.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

64. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi iliyotolewa na Mhe. Rais wakati wa Kampeni ya kumaliza mgogoro wa ardhi uliopo kati ya Wananchi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege KIA.

65. MHESHIMIWA ERICK JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaacha kuwatoza shilingi 600 wakati wa kuingia na kutoka Bandarini Wananchi wa Visiwa vya Kasalazi, Yozu, Gembela na Soswa katika Jimbo la Buchosa kwa kisingizio cha uwekezaji.

WIZARA YA MADINI:

66. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE MLAGHILA JUMBE (KYELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaufufua Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira;
- (b) Je, ni lini baadhi ya waliokuwa Wafanyakazi wa Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira watalipwa stahiki zao baada ya Mgodini huo kufungwa.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

67. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Maeneo ya Wananchi wa Kata ya Zinga Kitongoji cha Mlingotini na Pande yalichukuliwa na Serikali ili kupisha mradi wa EPZ lakini hawajalipwa fidia:-

Je, ni lini Wananchi hao watalipwa fidia.

68. MHESHIMIWA IRENE ALEX NDYAMKAMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuendeleza kilimo cha zao la miwa kwa Wananchi wa Wilaya ya Kalambo na Nkasi na baadae kujenga kiwanda cha sukari ambacho kitatoa ajira kwa Vijana na Wanawake ndani ya Mkoa wa Rukwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

DODOMA
13 APRILI, 2021

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE

